Da'wah As-Salafiyyah Ni Mwiba Wa Koo Kwa Khawaarij

Qur'an wa Sunnah Society of East Africa (QSSEA) www.qssea.net

DA'WAH AS-SALAFIYYAH NI MWIBA WA KOO KWA KHAWAARIJ

Mtayarishaji: Abu Farida Muhammad A. Basawad

NI NANI KHAWAARIJ:

Khawaarij ni pote ambalo lililojitokeza mwanzoni mwa utawala wa 'Alee (*Radhiallaahu 'anhu*). Walijitenga kutoka kwenye jeshi lake na wakaanzisha Uzushi mkubwa wa takfeer (Kuwafanya waislamu, watawala au raiya zake, kulingana na waonavyo wao kwa hatia ya kufanya madhambi makubwa, kuwa ni makafiri). Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) alituonya dhidi ya pote hilo katika ahaadeeth nyingi zilizo saheeh: "ma-Khawaarij ni mbwa wa motoni." Imepokewa na Ahmad na ni saheeh. Pia Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) alitupasha habari yakwamba wataendelea kujitokeza mpaka mwisho wa dunia hii, akisema, "Litajitokeza Pote wakiisoma Qur'aan, na wala haitopita koo zao, kila wakati pote hilo litakapojitokeza, likatiliwe mbali, mpaka atakapotokea ad-Dajjaal miongoni mwao."[1]

KUWAKUFURISHA WAISLAMU KWA AJILI YA KUFANYA DHAMBI

Amesema Aboo 'Abdullaah Ahmad ibn Hanbal (*Rahimahullaah*): "Na yeyote atakaeonana Nae (Allaah) baada ya kupitishwa juu yake *Hadd* kutokana na dhambi hilo (makhsusi) hapa duniani, basi hiyo itakuwa ndiyo kafara yake kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*).

Hii ni rai na madh-hab ya wanavyuoni wengi zaidi. Adhabu za kisheria zilizowekwa (*hudood*) ni kafara (za madhambi yaliyobainishwa) na hii ni kutokana na hadeeth ya 'Ubaadah ibn as-Saamit, itakayotajwa hapo mbeleni, apendapo Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) na ikapokewa na Bukhaaree na wengineo. Vilevile imetokana na hadeeth iliyopokewa na Imaam Ahmad katika Musnad yake, 5/214, kutoka kwa Khuzaimah ibn Thaabit, kwa mapokezi ya njia ya hassan ya riwaya hiyo, yenye maneno yafuatayo: "Yeyote afanyae dhambi kisha (adhabu za kisheria) zikatekelezwa juu yake (hapa duniani), basi hiyo itakuwa ndiyo kafara yake." Pia angalia maelezo kwa ukamilifu ya mas-ala haya kwenye *Fat-hul-Baaree* 1/64-68

Kutokamana na maneno yake (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) katika hadeeth ya 'Ubaadah, Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) alisema, walipokuwa kipote kidogo miongoni mwa maswahaba zake waliomzunguka, 'Kuleni kiapo cha Bai'ah kwangu (kwa yafuatayo): Yakwamba hamutomshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, yakwamba hamutoiba, yakwamba hamutofanya zinaa na kwamba hamutowauwa watoto wenu, na kwamba hamutokashifiana, baada ya kufanyiana njama miongoni mwenu, musi 'asi katika mambo mazuri na yaliyo na uadilifu. Yeyote miongoni mwenu atakaekufa (haliyakuwa amejiepusha na yote hayo) basi malipo yake ni kwa Mwenyezi Mungu, na yeyote atakaetumbukia katika jambo lolote miongoni mwa hayo, na akaadhibiwa hapa ulimwenguni, basi hiyo ndiyo itakuwa kafara yake. Na yeyote atakaetumbukia katika jambo lolote miongoni mwa hayo kisha Allaah akamkinga, basi hukmu yake itakuwa juu ya Mwenyezi Mungu. Akitaka Mwenyezi Mungu atamsamehe, na Akitaka Atamuadhibu.' Kwahivyo tukala kiapo cha Bai'ah juu ya hayo mbele yake."

[1] Imepokewa na Ibn Maajah na ni hassan. Angalia pia Silsilatul-Ahaadeethis-Saheehah (no. 2455)

Kwa hadeeth hii tunawakanusha *ma-Khawaarij* wenye kuwakufurisha *Waislamu* kwa ajili ya kufanya madhambi tu. Pia tunawakanusha pote la *Mu'tazilah*, wasemao yakwamba hapana shaka yakwamba mwenye kufanya madhambi ata-adhibiwa iwapo atakufa bila ya kutubia, na hii ni kwa sababu Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) hakusema yakwamba hapana shaka kuwa watu hawa wata-adhibiwa.

KUWAKUFURISHA WAISLAMU WATAWALA AU RAIYA

Yeyote mwenye kumu'asi kiongozi wa ki-Islamu ni miongoni mwa *ma-Khawaarij*, na amesababisha kutoafikiana miongoni mwa *Waislamu* na amekwenda kinyume na *Riwaya* Na anakufa kifo cha siku za ujinga (*Jaahiliyyah*).

Inajuzu kuwapiga vita *ma-Khawaarij* iwapo watawavamia watu, au mali, au jamii za *Waislamu*[2]. Lakini iwapo wataachana na hayo wakimbie basi hamuna haja ya kuwafurusha mbio, wala musiwauwe majeruhi wao, wala musiwaadhibu, wala mateka wao wasiuwawe, na muachane na waliokimbia.

'Abdullaah ibn al-Mubaarak amesema, "Mizizi ya mapote ya uzushi sabiini na mbili ni mapote manne: Na kutokamana na haya mapote manne, ndio kumechimbuka mapote sabiini na mbili. (Hayo mapote manne ni) *Qaadiriyyah*, *Murji'ah*, *Shi'ah* na *Khawaarij*[3]

Yeyote mwenye kumfadhilisha Abu Bakr, 'Umar, 'Uthmaan na 'Alee juu ya maswahaba waliobaki wa Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) na wala asiwazungumze maswahaba waliobaki isipokuwa kwa wema na akawaombea Mungu, basi huyo ameepukana na *Shi'ah*, mwanzoni mwake hadi mwisho wake.

Yule asemae kuwa Eemaan ni matamshi na vitendo na kwamba huzidi na kupungua, basi huyo ameepukana na Irjaa' mwanzoni mwake hadi mwisho wake.

Yule mwenye kusema yakwamba inajuzu kuswali nyuma ya kila (Imaam), mwema au muovu, na kwamba Jihaad na ipiganwe pamoja na kila Khaleefah na asihalalishe kumu'asi kiongozi kwa upanga na huwaombea Mungu (hao viongozi) ili Mwenyezi Mungu Awaongoze, basi huyo ameepukana na matamshi ya Khawaarij; mwanzoni mwake hadi mwisho wake. Huyo ni mtu wa Sunnah

Ama kwa yule asemae yakwamba kila kitu kinafanyika kwa *Qadar* ya Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*), mazuri na mabaya. Kwamba Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) humuongoza amtakae, basi huyo ameepukana na matamshi ya *Qaadiriyyah*; mwanzoni mwake hadi mwisho wake.

[2] Angalia Saheeh al-Bukhaaree (Eng, trans. Vol 9, UK. 49-53)
[3] Imepokewa na Ibn Battah katika Ibaanatul-Kubraa (No. 278)

JEE KUNA UMUHIMU WA KUJADILIANA NA WATU WA HIZBIYYAH?

Wanavyuoni wa ki-Salaf wanachukia sana kubishana (kwa hoja) na *watu wa Bid'ah* pamoja na kukaa nao. Kwa hakika wamekataza hata kuyataja au kuzinukuu shaka walizonazo kisha kuwafafanulia watu, na hayo ni kwa ajili ya kuhofia udhaifu wa yule mwenye kuyatumia, kutokuwa na uwezo wa kuyakanusha na kuyafanya kuwa ni mambo yasioleta manufaa na hatimae matokeo yakawa, yamemtia kwenye mitihani baada ya kuyasikiya au kuyasoma.

Katika haya kunapatikana kujihami katika nyoyo za Waislamu na ulinzi madhubuti wa fikra zao na fahamu zao. Hii pia ni mojawapo ya njia ya kuwafedhehesha na kuwadhalilisha *wazushi* na kizuizi dhidi ya rai zao na jeuri walizonazo kwa kutotumia vitabu vya *Salaf* wanapozitathmini rai zao za upotofu. Miongoni mwa riwaya (kuhusiana na *Wazushi*) kutoka kwa *Salaf* zenye kubainisha mifumo yao ni kama yafuatayo:

Alivyosema Sufyaan ath-Thawree (*k. 161H*), "Yeyote atakaesikia jambo la uzushi, basi asiwaarifu rafiki zake kuhusiana na uzushi huo (ili) asije akawavurumizia wenzake (*ya uzushi*) katika nyoyo zao (yaani mambo hayo yakawaathiri)[4]

Ayyoob as-Sakhtiyaanee akasema (*k. 131H*), "Hakuna jambo lenye kuwakera mno munapowakanusha uwongo wao zaidi ya kuwanyamazia (yaani; musifanye mijadala nao).[5]

Ibn Battah (*k. 387H*) akapokea kutoka kwa 'Abdullaah ibn as-Sariyy aliyesema, "Si Sunnah kwetu sisi, kufanya mijadala ya mizozo na watu wa *Hawaa'*, lakini Sunnah kwetu sisi ni kwamba hatuzungumzi na hata mmoja wao.[6] Vile-vile akapokea kutoka kwa Hanbal ibn Ishaaq ibn Hanbal yakwamba amesema, "Mtu Fulani aliandika kitabu kisha akampelekea Aboo 'Abdillaah (Imaam Ahmad) (*Rahimahullaah*) akitarajia kupata ruhusa kutoka kwake ya kukiandika kitabu hicho ambacho ndani yake muna maelezo kuhusu ukanushaji dhidi ya *watu wa Bid'ah* na mapambano na watu wenye ufasaha wa mazungumzo (*Ahlul-kalaam*) kubishana nao na kuwasilisha hoja kwao. Kwahivyo Aboo 'Abdullaah akamuandikia yeye kitabu na akasema ndani yake yakwamba: "Yale ambayo tulokuwa tukiyasikia na kuwakuta nayo watu wenye Ilimu kuwa wameshikamana nayo, ni kwamba walikuwa wakichukia kuzungumza na kukaa na *Watu Wapotofu*. Shauri letu ni kujitegemeza kwa unyenyekevu na kukomeka na kila kilichomo kwenye kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume wake (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*), wala sio kukaa na *watu wa upotofu na uzushi*, kwa min-ajil ya kuwakosoa, kwani wao watakurengesha haliyakuwa wao wenyewe hawatorudi nyuma. Kwahivyo usalama, apendapo Mwenyezi Mungu, unapatikana kwa KUPIGA MARUFUKU KIKAO NA WAO NA KUTOBISHANA NAO KUHUSIANA NA UZUSHI WAO.

Ma'mar akasema, "Mtoto wa Taawoos (*k. 104H*) alikuwa amekaa, mara jamaa mmoja miongoni mwa *Mu'tazilah* akatokea kwenye kikao hicho na akaanza kuzungumza.

[4] Sharhus-Sunnah ya Imaam al-Baghawee, (1/227)
[5] Al-Ibaanah cha Ibn Battah, 2/365-366.
[6] Al-Ibaanah cha Ibn Battah, 2/365-366

Taawoos akatia vidole vyake ndani ya masikio yake na akasema, "Ewe mwanangu! Ingiza vidole vyako ndani ya masikio yako ili usiyakisize hayo ayasemayo huyo, kwani huu moyo ni dhaifu (yaani; moyo wa mwanae). Kisha akasema, 'Ewe mwanangu! Tia vidole vyako KWA NGUVU, KWA NGUVU.' Na akaendelea kutamka neno hilo bila ya kunyamaza, 'KWA NGUVU,' mpaka yule jamaa akasimama na kuondoka kutoka kwenye kikao hicho.[7]

Kwa hakika leo kuna wengi wenye kusema, *Walhamdulillaah,* kuhusu Qur'aan na Sunnah na kujinasibisha nazo. Hatahivyo, kuwajibika tunakolingania sisi sio katika kuandika maneno matupu hapa na kutowa darasa pale, khaswa makusudiwa yetu ni kwamba Qur'aan na Sunnah yafanywe kuwa ndio mfumo kwa ujumla juu ya kila jambo, kubwa au dogo na kwamba *manhaj* zifanywe kuwa ndio nguo zao za ndani na nje za *Da'wah* – Kuanzia mwanzo hadi mwisho na kwamba fikra za wale vijana na wenzao wenye kufanya hii shughuli ya *Da'wah* iongozwe kulingana na hii *manhaj* tukufu, ambayo juu yake ndipo upatikanapo ufanisi wa *Ummah*.

[7] Imepokewa na Imaam al-Laalikaa'ee katika Sharh Usoolul-I'tiqaad, No. 248 kwa tafauti ya maneno.